**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 2, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mdhihirisho wa Mahusiano ya Uwezo katika Vikatuni vya Shujaaz: Uchanganuzi Makinifu wa Kidiskosi

*Sammy Liana Dimbu*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Chuka, S. L. P. 109 - 60400, Chuka, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0001-5070-6915; Barua pepe ya mawasiliano: dimbuliana@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*08 Novemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Diskosi, Shujaaz, Mahusiano ya Uwezo, Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi, Vikatuni na Vijana.*

**IKISIRI**

Vikatuni ni chombo muhimu cha mawasiliano katika Karne ya 21. Huenda ndio sababu vimeendelea kukumbatiwa katika uwasilishaji wa masuala yanayohusu vijana. Makala hii inahusu Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi katika vikatuni vya Shujaaz ili kubainisha uzalishaji wa mahusiano ya uwezo katika vikatuni hivi. Utafiti huu ni wa kiisimu na ni hatua kutokana na tafiti tangulizi zilizotafitia vikatuni hivi katika taaluma ya fasihi. Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi iliongoza utafiti huu. Kwa mujibu wa nadharia hii changamoto za kijamii hubainika katika uzalishaji wa matumizi mabaya ya mamlaka au udhalimu wa wenye mamlaka katika diskosi. Data ya makala hii ilitokana na sampuli ya nakala 35 za diskosi ya Shujaaz zilizoteuliwa kimakusudi kwa kuzingatia kigezo cha yaliyomo. Mpango wa kimaelezo ulitumika katika kuchanganua na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Matokeo ni kuwa mahusiano ya uwezo katika Shujaaz ni baina ya: wahusika mashujaa na wahusika wa kawaida, wahusika mashujaa na vijana, wadhamini na vijana, hadhira lengwa ambao ni vijana na mtu mashuhuri na mahusiano ya uwezo ya kiuana. Makala hii inatoa mchango katika taaluma ya isimu kwa kubainisha namna mahusiano ya uwezo yanavyotumiwa kuangazia masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, na namna yanavyoweza kutumiwa kuwashirikisha vijana katika masuala yanayowakumba katika jamii. Utafiti huu unapendekeza tafiti zaidi za baadaye zifanywe kwa kuzingatia mikakati ya uhalalishaji na uharamishaji inayodhihirika kupitia mahusiano ya uwezo katika diskosi ya Shujaaz.

**APA CITATION**

Dimbu, S. L. (2022). Mdhihirisho wa Mahusiano ya Uwezo katika Vikatuni vya Shujaaz: Uchanganuzi Makinifu wa Kidiskosi. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 40-57. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

**CHICAGO CITATION**

Dimbu, Sammy Liana. 2022. "Mdhihirisho wa Mahusiano ya Uwezo katika Vikatuni vya Shujaaz: Uchanganuzi Makinifu wa Kidiskosi". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 40-57. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946.

**HARVARD CITATION**

Dimbu, S. L. (2022) "Mdhihirisho wa Mahusiano ya Uwezo katika Vikatuni vya Shujaaz: Uchanganuzi Makinifu wa Kidiskosi", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 40-57. doi: 10.37284/jammk.5.2.946.

**IEEE CITATION**

S. L. Dimbu, "Mdhihirisho wa Mahusiano ya Uwezo katika Vikatuni vya Shujaaz: Uchanganuzi Makinifu wa Kidiskosi", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 40-57, Nov. 2022.

**MLA CITATION**

Dimbu, Sammy Liana. "Mdhihirisho wa Mahusiano ya Uwezo katika Vikatuni vya Shujaaz: Uchanganuzi Makinifu wa Kidiskosi". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Nov. 2022, pp. 40-57, doi:10.37284/jammk.5.2.946.

## UTANGULIZI

Diskosi hurejelea lugha na mitazamo ya kitamaduni. Hivyo ni mwingiliano baina ya lugha, matendo, mitagusano, fikira, imani na matumizi ya ishara ili kujenga ujitambulishaji wa jamii (Gee, 2005), kama vile "shujaa", "wafadhili" na "vijana". Kinachofanya uchanganuzi wa diskosi kuwa makinifu ni namna lugha inavyozalisha na kuendeleza utawala dhidi ya watawaliwa na matumizi mabaya ya mamlaka; dhuluma na ubaguzi (van Dijk, 2001). Uwezo ni watu kumtii mwengine kwa hiari bila ya kushurutishwa. Watu wenye hadhi ya juu kuliko wengine katika makundi mbalimbali ya kijamii hutumia lugha kama dhihirisho la uwezo. Ina maana kuwa *Shujaaz* hushadidia itikadi zinazotawala jamii nchini Kenya na itikadi hizi hukuza na kuendeleza mahusiano ya uwezo yasiyokuwa sawa baina ya wadau mbalimbali katika jamii.

Data ya makala hii ilitokana na jarida la vikatuni vya *Shujaaz* linalowasilishwa kwa msimbo wa Sheng. "Shujaaz" ni istilahi yenye maana sawa na dhana "mashujaa" katika Kiswahili Sanifu. Kwa mujibu wa McCloud (1993), dhana ya vikatuni ni michoro ya picha iliyopangwa pamoja katika msuko ili kupitisha maarifa au kuzua ujumi. Fasili hii haijakamilika kwa sababu ilitenga vikatuni vinavyowasilishwa kwa michoro ya picha iliyoambatishwa maandishi. Hata hivyo mjadala kuhusu dhana hii kulingana na Boyd (2015), husheheni hoja tatu: Kwanza, msuko; michoro ya picha zilizopangwa kwenye paneli zaidi ya moja ili kujenga mtiririko wa hadithi. Msuko ndicho kipengele kikuu cha kuwepo kwa tofauti iliyopo baina ya vibonzo na vikatuni. Vibonzo husimulia hadithi kwa paneli moja ilhali msuko wa vikatuni hukuzwa kwa paneli mbili au zaidi. Pili, michoro ya picha; vikatuni lazima viwe na michoro ya picha. Michoro hii hupambanua maana ya maandishi panelini. Hatimaye, maandishi hukamilisha vikatuni kwa sababu ni kipengele kinachoendeleza mwingiliano baina ya michoro ya picha na msuko wa hadithi (Nortion, 2003).

Jarida la *Shujaaz* huchapishwa na kampuni ya *Well Told Story* kuanzia Februari, 2010 mara moja kwa mwezi. Ndani mna michongoano, hotuba, tawasifu, habari kutoka mitandao ya kijamii na tamthilia inayoigizwa kwa njia ya michoro ya picha. Malengo makuu ya jarida hili ni kuburudisha na kuwaelimisha vijana kuhusu uongozi, kuanzisha na kuendeleza biashara, elimu ya afya ya uzazi na kilimo. Jarida hili hutolewa bure. Wahusika wakuu katika *Shujaaz* ni; Dj Boyie, Charlie Pele, Malkia na Maria Kim. Ushujaa wa wahusika hawa hutokana na juhudi zao za kubuni mbinu za kusuluhisha changamoto zinazowakumba vijana katika uhalisia wa maisha yao. Ni kutokana na jarida hili kuwasilishwa kwa lugha ya kutazamwa ambayo ni zao la uchoraji wa michoro ya picha na uandishi ndipo lilifaa kutafitiwa kiisimu. Mada ya makala hii iliangaziwa kupitia sehemu zifuatazo: anwani, ikisiri, utangulizi, historia ya vikatuni, mbinu za utafiti, uchambuzi wa data, hitimisho na marejeleo.

### Historia ya Vikatuni

Usuli wa mfumo wa ukuaji wa muundo wa vikatuni ulimwenguni unahusishwa na kuvumbuliwa kwa taaluma ya uchapishaji (McCloud, 1993). Mwanzo wa uchapishaji wa vikatuni ulimwenguni kama anavyosimulia Scott (2011) unahusishwa na Mwingereza Willam Hoggarth. Kutokana na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

vikatuni vya kukejeli vilivyochapishwa katika machapisho sita mnamo mwaka wa 1731. Machapisho yaliyosomwa kwa awamu. Raia wa Uswizi Rodolphe Topffer mnamo mwaka wa 1840 aliambatisha maandishi na michoro ya picha. Hali hii ilikuwa kichocheo kikubwa katika kuafikia muundo wa sasa wa vikatuni.

Ulimwenguni vikatuni vilichapishwa nchini Japan na Marekani kwa mara ya kwanza katika Karne ya 18 na 20 mtawalia (Scott, 2011). Mmarekani Wertham (1954) anaeleza kuwa vikatuni vilishinikiza fujo na ubaguzi wa kijinsia miongoni mwa vijana na watoto. Haya ni masuala ambayo yalidhihirika katika data ya utafiti huu na kupitia kwake mahusiano mbalimbali ya uwezo yalikuzwa na kuendelezwa. Mtazamo huu wa Wertham (Keshatajwa) ulidumaza ukuaji na msambao wa soko la vikatuni nchini Marekani na New Zealand. Pia, kilikuwa kisababishi kikuu cha kuundwa kwa kamati ya Bunge la Senati nchini Marekani iliyochunguza madai haya. Kamati hii ilikusudiwa kutathmini masuala yaliyofaa kuchapishwa katika vikatuni. Kampuni za uchapishaji baadaye zilijitungia kanuni ili kudumisha imani ya jamii (Nyberg, 1998), katika vikatuni. Kanuni hizi zililenga kuendeleza thamana ya ujumbe uliohalalishwa kuchapishwa.

Barani Afrika vikatuni vya kwanza kuchapishwa vilitoka mataifa ya Kimagharibi (Lent, 2009) na mtindo wa uchoraji ulikuwa wa aina moja. Vyombo vya habari vilipiga chapa vikatuni vya mataifa waliyotoka wakoloni. Vichache vilichapishwa na walowezi na wamishenari. Majarida ya wamishenari yalipuuza vikatuni kwa sababu vingeshusha hadhi ya habari za injili. Vichache vilivyochapishwa vilikosa umaarufu kwa sababu ya kukosa kuangazia mada zenye ucheshi na ngono (Jigal, 2006).

Hata hivyo vikatuni vilivyochapishwa baada ya uhuru vilisheheni wahusika na mandhari ya Kiafrika. Afrika Mashariki vikatuni vilichapishwa kwa mara ya kwanza katika kipindi kinachokaribia mwaka wa 1907 na gazeti la kikoloni la *The Standard* (Beck, 1999). Vikatuni vilivyochapishwa katika kipindi hiki ni pamoja na; *Andy Capp, Eband, Flo* na *Popeye*. Vikatuni vya asili katika Afrika Mashariki vilichorwa na Edward Ngure Gitau (Otuoma, 2015). Anavyosema Otuoma (keshatajwa) ni kuwa vikatuni hivi vilichapishwa katika mwongo wa 1950 chini ya anwani *Juha Kalulu* na vilichapishwa rasmi mnamo mwaka wa 1973 na gazeti la burudani la *Joe* (Beck, 1999).

Licha ya ukweli kuwa vikatuni vina historia ndefu, havijatafitiwa kwa mapana na marefu katika nyanja za usomi (Dittmer, 2005). Vikatuni vinavyochapishwa Barani Afrika vimepuuzwa kwa muda mrefu kwa sababu ya baadhi ya wataalamu kuwa na mitazamo hasi. Kwa mfano, Lanternari (1970) anasema kuwa ni nadra sana kupata vikatuni na ucheshi katika jamii zenye sanaa shenzi. Hivyo wasomi kutoka mataifa ya Kimagharibi katika miaka ya 1960 waliichukulia sanaa ya Kiafrika kuwa shenzi na iliyokosa vikatuni (Jigal, 2006). Hata hivyo ukuaji wa tafiti katika kipindi cha hivi karibuni ni ithibati kuwa dhima ya vikatuni si kuburudisha tu bali ni pamoja na kukuza mawasiliano, kuelimisha, kuzindua hadhira lengwa na kutoa maarifa mbalimbali.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Viongozi wa kiimla katika historia ya binadamu huwadhibiti, huwatimua au hata kuwaua wanavibonzo wanaowakejeli (Scott, 2007). Mtaalamu Otuoma (2015), alitafitia uchanganuzi wa mtindo na maudhui katika vibonzo vya mhariri katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti wake ulibainisha kuwa vibonzo vya mhariri huwasilishwa kupitia kejeli, kinaya, na jazanda. Maudhui ya ufisadi, ukabila, ukosefu wa usalama, elimu, uchumi na kazi na siasa hutamalaki. Mahusiano ya uwezo yalidhihirika kupitia maudhui kama vile ufisadi, ukabila, elimu, uchumi na siasa. Utafiti wa Otuoma (keshatajwa), ulifaa makala hii katika kueleza hatua za kufafanua mahusiano ya uwezo katika paneli kulingana na muktadha wa kijamii. Sampuli ya utafiti wa Otuoma (keshatajwa), imetokana na gazeti la *Taifa Leo* ilhali sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kutoka jarida la *Shujaaz.*

Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi hutoa sababu zinazofanya diskosi kukubaliwa katika jamii jinsi zilivyo (Fairclough, 1995). Msimbo wa Sheng hutawala diskosi za vijana na watoto katika viwango vyote vya elimu kuanzia chekechea, msingi, sekondari na vyuo vikuu (Githiora, 2002). Naye Ngugi (2017), alitafitia fasihi katika lahaja ibukizi, mifano kutoka chapisho la *Shujaaz*.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Aliangazia jarida hili kama nyenzo ya kusomwa kifasihi. Baadhi ya maudhui katika *Shujaaz* ni pamoja na: uwajibikaji na kuhimiza vijana kutia bidii maishani. Utafiti wa Ngugi umefaa katika kutathmini ni kwa namna gani baadhi ya maudhui yalivyokuza dhamira ya jumla katika diskosi ya *Shujaaz*. Hata hivyo uliegemea taaluma ya fasihi ilhali makala hii inajikita kwenye taaluma ya isimu katika kiwango cha Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi hususani mahusiano ya uwezo.

Lugha kama chombo kinachounda jamii haiwezi kujitenga na itikadi (van Dijk, 1998). Nao Sardabi, Biria na Azin (2014), walitafiti kuhusu hotuba ya Rais wa nchi ya Iran, Hassan Rouhan katika mkutano wa 68 wa Baraza la Umoja wa Mataifa mnamo mwaka wa 2013. Waligundua kuwa Rais Rouhan alikuwa na mtazamo tofauti akilinganishwa na Marais waliomtangulia katika Taifa hilo. Rais Rouhan alijiwasilisha kuwa bora kuliko Marais waliomtangulia kuhusu uhusiano wa nchi ya Iran na mataifa ya Kimagharibi. Utafiti wa Sardabi, Biria na Azin (keshatajwa) ulifaa utafiti huu katika kueleza namna makundi yenye uwezo huwasilisha maslahi yao kupitia *Shujaaz* ili kueneza itikadi yao. Makala hii ni tofauti na utafiti wa Sardabi, Biria, na Azin (keshatajwa), kwa sababu sampuli ya utafiti wao ilihusu hotuba ya Rais Rouhan katika mkutano wa 68 wa Baraza la Umoja wa Mataifa.

## MISINGI YA NADHARIA

Makala hii iliichukulia diskosi ya *Shujaaz* kama uwanja uliodhihirisha mapambano ya kunyakua mamlaka baina ya wadau mbalimbali katika jamii. Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi hudokeza kuwa diskosi na jamii hutegemeana na kujengana. Waasisi wa nadharia hii ni pamoja na Fairclough na Wodak (1997). Nadharia hii hutoa sababu zinazofanya diskosi ambazo ni zao la jamii kukubaliwa jinsi zilivyo (Fairclough, 1995). Kwa mujibu wa Fairclough (1992) Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi unaweza kutokea kwa namna tatu. Kwanza, Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi hujikita kwenye vipashio vya kiisimu kama vile leksimu, sarufi, muwala na muundo wa diskosi. Mtazamo huu ulifaa makala hii kueleza namna istilahi maalumu zilivyodhihirisha mahusiano ya uwezo. Pili, uchanganuzi unashughulikia diskosi kama mchakato wa kijamii. Hii ina maana kuwa diskosi ni mali ya jamii na hutekeleza wajibu wake kutegemea matarajio ya wanajamii ambamo diskosi hiyo imezalishwa. Matarajio haya huwa sehemu muhimu ya maarifa ya kiusuli yanayokuza mahusiano ya uwezo.

Hatimaye, diskosi ya *Shujaaz* ilishughulikiwa kama suala la mazoea ya kijamii. Mtazamo huu ulifafanua namna diskosi huzaliwa, husambazwa, huenezwa na kutumiwa katika jamii. Mikakati mbalimbali ya mazoea ya kijamii ilitumiwa kuipa diskosi hii utambulisho katika mazingira ya kijamii inamosomwa na huendeleza mahusiano ya uwezo.

Mihimili iliyoongoza makala hii ni pamoja na: diskosi huundwa na jamii, matumizi ya lugha huamuliwa kijamii na lugha hubadilika kulingana na hali ya jamii, diskosi husaidia katika kuunda na kubadilisha maarifa, mahusiano ya jamii na utambulisho wa jamii, diskosi huundwa na mahusiano ya uwezo na husheheni itikadi. Mhimili huu hudokeza athari za kijamii katika diskosi. Mihimili hii ilifaa katika kuchanganua *Shujaaz* kama mali ya jamii na matumizi ya Sheng katika uwasilishaji wake yalichangiwa na mabadiliko ya jamii. Aidha kueleza kuwa diskosi hii husheheni maarifa ya jamii na huendeleza ujitambulishaji miongoni mwa vijana unaoamuliwa na mahusiano ya uwezo katika jamii inamosomwa.

## MBINU ZA UTAFITI

Makala hii ilitumia mpango wa kimaelezo katika kuchanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Usampulishaji katika makala hii ulikuwa mchakato wa kuteua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la nakala za *Shujaaz* zilizotafitiwa ili kuyaafikia malengo ya utafiti (Kothari, 2009). Kwa mujibu wa Gay (1992), mtafiti huteua sampuli kwa sababu ya kuwepo kwa ufinyu au udhaifu fulani ambao huzuia kutafitia idadi lengwa yote. Ufinyu na udhaifu uliomkumba mtafiti unafafanuliwa na Mugenda na Mugenda (1999) wanapoeleza kuwa rasilimali na wakati ndivyo vizuizi vikubwa katika kufanya maamuzi kuhusiana na uteuzi wa sampuli. Mtafiti aliteua kimakusudi jumla ya nakala 35 za jarida la *Shujaaz* kwa kuzingatia kigezo cha yaliyomo. Mugenda na Mugenda (keshatajwa) wanaeleza kuwa katika mbinu ya kimakusudi, mtafiti huwa na uhuru wa kuteua sampuli zilizo na data iliyohitajika. Mtafiti aliteua nakala moja kwa kila matoleo matatu, kuanzia toleo la kwanza

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

Februari, mwaka wa 2010 hadi toleo la Disemba, mwaka wa 2018.

## MATOKEO

### Wahusiano ya Uwezo katika Vikatuni vya *Shujaaz*

Makala hii iliangazia vipengele vinavyokuza mahusiano ya uwezo kupitia vijimada mbalimbali. Hivi ni pamoja na: mahusiano ya uwezo baina ya: wahusika mashujaa na wahusika wa kawaida, wahusika mashujaa na vijana, yaani hadhira lengwa, wadhamini wa jarida la *Shujaaz* na vijana, hadhira lengwa ya vijana na mtu mashuhuri na mahusiano ya kiuana.

### Mahusiano ya Uwezo baina ya Wahusika Mashujaa na Wahusika wa Kawaida

Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa kuna mahusiano ya uwezo baina ya wahusika mashujaa na wahusika wa kawaida. Kutambulika kwa mhusika ni sifa ya kimsingi ya vikatuni (Mikkonen, 2017). Wahusika mashujaa katika jarida la *Shujaaz* ni pamoja na: DJ Boyie, Charlie Pele, Malkia na Maria Kim. Kwa mfano, katika *Shujaaz* #39, ukurasa wa 18-23, Maria Kim alipopokea habari kuwa mdogo wake Brayo alimrushia mhusika Mama Stacey jiwe. Shujaa Maria Kim alitafuta maoni ya wanajamii kuhusu vijana waliopotoka kimaadili. Tazama:

**Kielelezo 1: Shujaaz chapta #39, ukurasa wa 21**




Paneli ya kwanza Maria Kim aliambiwa na mhusika wa kike:

> *Kijana yangu alikuwa mzuri. Lakini alijoin gang, wakaanza kutumia madawa za kulevya… siku hizi hata sijui ako wapi.*

> *Kijana (mvulana) wangu alikuwa (mwenye tabia) mzuri. Lakini alijiunga na kikundi chenye sifa mbaya na wakaanza kutumia dawa za kulevya… hata sijui aliko siku hizi.*

Mhusika Maria Kim alitarajiwa kutafuta suluhu ya vijana kujiunga na matumizi ya dawa za kulevya.

Paneli ya pili, mhusika aliyeketi barazani anamwambia Maria Kim:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

> *Josphat alisoma mpaka class 8. Alikataa kwenda form 1 siku hizi anarandaranda tu. Mimi husikia ni mwizi.*

> *Josphat alisoma hadi darasa la nane baadaye alikataa kujiunga na kidato cha kwanza. Siku hizi yeye hurandaranda tu. Mimi husikia ni mwizi.*

Maria Kim aliambiwa nukuu hii kwa matarajio kuwa angepata suluhu dhidi ya visa vya vijana kuacha shule na kushiriki wizi.

Paneli ya tatu mhusika wa jinsia ya kike anayeuza nyanya anamwambia Maria Kim:

> *Natamani Jemimah angekuwa kama wewe. Yeye hulewa kila wakati! Sasa nitasaidia huyo msichana yangu aje?*

> *Ninatamani Jemimah angekuwa (na hulka njema) kama wewe. Yeye hulewa kila wakati! Sasa nitamsaidia msichana wangu vipi?*

Paneli hii ilimsawiri Maria Kim kama shujaa ambaye angeikomboa jamii kutokana na visa vya vijana kujiunga na uraibu wa kunywa pombe.

Paneli ya nne mzee katika gari la matatu anasema:

> *Siku moja nikapita hii street usiku nikaona msichana yangu kumbe she sells her body! My daughter.*

> *Siku moja nilipita barabara hii usiku nikamwona mwanangu kumbe anauza mwili wake (ni kahaba)! binti yangu.*

Mhusika huyu analalamika kuhusu mwanawe kuwa kahaba. Kwa matarajio kuwa Maria Kim angepata suluhu ya visa vya wasichana kushiriki ukahaba.

Kwa mujibu wa Phillips na Strobl (2006) uhalifu vikatunini hutokea kupitia matumizi ya nguvu za kimabavu na dawa za kulevya. Kwa mujibu wa paneli hizi vijana hutumia dawa za kulevya na pombe, hukataa masomo na hushiriki ukahaba. Lugha inapotumika na wale wenye taaluma tajika, tabaka la juu na nyadhifa za kisiasa kwa kawaida hutawala mfumo wa mtagusano katika jamii (Fairclough, 1989). Mhusika Maria Kim alitawala mkakati wa kutafuta suluhu ya vijana wanaojiunga na makundi ya uhalifu.

Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi huelezea dhana ya uwezo kama kundi la watu ambalo hudhibiti shughuli mahususi ya mawasiliano. Hadhi ya Maria Kim ya kuwa shujaa ilimpa mamlaka ya kushinikiza wahusika wengine ili kuyaafikia malengo yake. Wahusika katika vikatuni vya mashujaa huwa na nafasi bora ya kuangazia mema dhidi ya maovu katika jamii (Kading, 2005). Hali hii imewekwa bayana kupitia mazungumzo baina ya wahusika Maria Kim na JK katika *Kielelezo 2*.

**Kielelezo 2: Shujaaz chapta #39, ukurasa wa 20**




> *Maria Kim: Ninaogopa hata Brayo ataingia life ya uhalifu. Ninaogopa hata Brayo atajiunga na uhalifu.*

> *JK: Usigive up, I'm sure tunaweza get solution. Ninajua wewe. Ninajua uta-get idea ya kuwasaidia. Usife moyo, ninaimani tutapata*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

*suluhu. Ninajua utapata wazo la namna ya kuwasaidia.*

Panelini mhusika JK anaamini kuwa Maria Kim angeikomboa jamii kutokana na hali ya vijana kujiunga na makundi ya kiuhalifu. Baadaye Maria Kim alipigania haki za vijana katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na bunge la gatuzi. Hatimaye, umati wa wanajamii uliamua kushirikiana naye kwa kuunga mkono juhudi zake za kuwaepusha vijana na uhalifu. Mhusika Mama Stacey aliyeongoza umati huu katika *Kielelezo 3*, anasema:

**Kielelezo 3: Shujaaz chapta #39, ukurasa wa 23**




*Mama Stacey: Tumefika! Tume-come ku-support hiyo idea yako. Tunajua ni ya maana sana!*

*Tumefika! Tumekuja kuunga mkono hilo wazo lako. Tunajua ni la manufaa sana!*

Kwa mujibu wa Dittmer (2005) adui wa shujaa katika vikatuni ni adui wa jamii. Mhusika Maria Kim ni kiongozi aliyepinga hulka ya vijana kujiunga na makundi ya uhalifu. Kwa mujibu wa Boyd (2015) aghalabu vikatuni huwa uwanja wa mapambano ya mema dhidi ya maovu. Hivyo mhusika Maria Kim aliwakilisha waliopinga uhalifu na kukuza umoja na ujitambulishaji baina ya wanajamii ambao ni wafuasi wake.

## Mahusiano baina ya Wahusika Mashujaa na Vijana

Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa kuna mahusiano ya uwezo baina ya wahusika mashujaa na vijana. Wahusika mashujaa ni mfano bora unaopaswa kuigwa kwa hadhira lengwa. Matendo na lugha ya mashujaa katika mitagusano yao na hadhira si chombo bia cha mawasiliano. Aghalabu husheheni maslahi ya makundi yenye uwezo katika kushinikiza mipango, maslahi na ajenda fulani katika jamii husika (Alvi na Baseer, 2012). Tazama mfano paneli ifuatayo, *Kielelezo.4* mhusika shujaa, Malkia aliwaelimisha vijana kuhusu namna ya kuzuia mifugo kuharibu mimea shambani:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

**Kielelezo 4: Shujaaz chapta #17, ukurasa wa 12**




Katika paneli ya kwanza, Malkia alipata wazo kuhusu namna ya kuzuia mifugo kuharibu mimea. Mchoro wa taa uliyopo juu ya kichwa cha Malkia unawakilisha wazo lenye manufaa ambalo limemjia akilini kwa ghafla. Mhusika Malkia kutazamana na msomaji inadokeza kuwa matukio katika paneli zinazofuata ni kwa manufaa ya msomaji. Paneli ya pili, ina maneno ya mwandishi "chukua mbolea ya mbuzi" (chukua samadi ya mbuzi) weka kwenye ndoo. Paneli ya tatu, msomaji alishauriwa aunde mchanganyiko wa maji na samadi. Hatimaye, apake mchanganyiko huo kwenye majani ya mimea. Paneli zilizofuata mbuzi wanapokaribia mimea iliyopakwa mchanganyiko huu na kujaribu kula, wanashindwa.

Hatua baada ya nyingine vijana wanaelimishwa namna ya kuzuia mifugo kuharibu mimea. Kwa mujibu wa Nesler na wengine (1991), imani, maarifa na maoni hupokelewa na kuaminika katika diskosi kutokana na kile wapokeaji wanachokiona kuwa na mamlaka yanayotokana na wasomi, wataalamu au vyombo vya habari vya kuaminika. Ni matarajio ya mwandishi kuwa vijana wakulima wangeiga namna ya kuzuia mifugo kuharibu mimea shambani kutokana na mafunzo panelini.

**Mahusiano baina ya Wadhamini na Vijana**

Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi huchunguza diskosi ili kubainisha namna miundo, mikakati au vipengele vingine vya usemi, mazungumzo au matukio ya mawasiliano yanavyotekeleza wajibu wake katika uzalishaji wa mahusiano yasiyokuwa na usawa (Fairclough na Wodak, 1997). Wadhamini katika vikatuni vya *Shujaaz* huwa na uwezo wa kiuchumi kuliko vijana. Hali hii inawapa mamlaka ya kudhibiti na kushinikiza matendo ya vijana katika jamii vinamosomwa vikatuni hivi. Uwezo huu unatokana na wao kuwa na rasilimali inayowawezesha kudhibiti uwasilishaji wa maslahi yao katika diskosi ya *Shujaaz*.

van Dijk (2008), anadai kuwa Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi hutumiwa kutathmini maana ya umaanisho kuhusu ubaguzi wa rangi, nafasi ya kitabaka na hejemoni. Kwa mujibu wa Fairclough (1995) hejemoni ni namna mamlaka ya kundi tawala yanavyokubaliwa na kuhalalishwa kupitia sheria, tambiko za jamii, mawasiliano na hulka. Wasomi wa Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi huitazama hejemoni kuwa njia ambayo fikira na matendo hukubaliwa katika jamii (Fairclough, 1989). Hejemoni ya wafadhili katika diskosi ya


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

*Shujaaz* ilitamalaki kwa sababu ya vijana kukosa uwezo wa kuamua kinachochapishwa. Hejemoni hii ilisheheni namna michakato ya mazoea ya kijamii yalikuwa sehemu ya mchakato mpana wa kijamii na kitamaduni na namna ilifaa katika kuhimidi hali za kijamii inamosomwa diskosi hii. Uwezo ambao huenda wadhamini wanao. Aidha, vijana huenda walikosa maarifa na imani iliyohitajika kupinga diskosi au maslahi ya wadhamini.

Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ni uchanganuzi wa miktadha mbalimbali ya mitagusano ya jamii kwa minajili ya kuweka wazi namna matumizi ya lugha husheheni itikadi na mahusiano ya uwezo (Fairclough na Wodak, 1997). Jarida la *Shujaaz* ni jukwaa ambalo wadhamini kwa njia iliyofiche hutangaza bidhaa, huduma na kueneza hejemoni ya itikadi yao. Itikadi hii hupata mamlaka na uhalalishaji wake kutokana na kibali cha hiari wala si kwa nguvu. Uhalalishaji huu husheheni mfumo ambao jarida hili hutoa leseni ya vijana kushabikia maslahi ya wadhamini. Kwa mujibu wa Eagleton (1991), itikadi ni maslahi ya kundi mahususi la watu na hurejelea mawazo na imani inayoashiria hali na tajriba ya kundi mashuhuri au tabaka la juu. Hivyo vijana ambao ni hadhira lengwa hawana budi ila kusoma hadithi iliyosheheni maslahi ya wadhamini. *Kielelezo 5* kina michoro ya nyumba zilizo na nembo ya kampuni ya *Safaricom*. Tazama:

**Kielelezo 5: Shujaaz chapta #39, ukurasa wa 3**




Panelini nembo ya kampuni ya mawasiliano ya simu ya *Safaricom* nchini Kenya iko kwenye michoro ya nyumba. Imani iliyorithishwa na tangazo hili ni kuwa kampuni ya *Safaricom* ilihusishwa na umati wa watu. Nyumba panelini zinakaribiana na mkutano wa baraza la chifu ambalo huenda lingehudhuriwa na umati wa watu. Tangazo hili liliazimia kuwashawishi vijana kukubali umaarufu wa huduma za *Safaricom*.

Kwa mujibu wa Raskin (2008), vikatuni hutumika kuficha hisia halisi na imani kwa sababu huficha kile ambacho hakiwezi kusemwa hadharani. Vikatuni vinavyorejelea kinachosemwa kwa uwazi, havina mashiko na havitekelezi wajibu uliokusudiwa. Nembo hii ilitangaza na kuhalalisha maslahi ya kampuni ya *Safaricom* kwa uwazi dhidi ya maslahi ya kumpuni nyingine pinzani. Maslahi ya kampuni pinzani yaliharamishwa kutokana na nembo zao kutokuwepo panelini. Japo si kwa njia ya moja kwa moja. Wanavyosema Ivan na Clark (1997), ni kuwa watu hawapati maana katika ombwe tupu. Matumizi ya lugha husheheni muktadha wa kijamii. Muktadha wa kimazingira panelini ni nchini Kenya na lengo la nembo hii ya kampuni ya *Safaricom* katika diskosi ya *Shujaaz* ni fiche.

Hii ni kwa sababu lengo la nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ni kubainisha mwingiliano na mahusiano yaliyofiche ili yasionekane na watu (Fairclough, 1995). Nadharia hii inajihusisha na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

mahusiano baina ya matumizi ya diskosi na uwezo. Kuwepo kwa istilahi *Safaricom* ni njia mojawapo ya kujenga hejemoni katika soko la huduma za mawasiliano. Kwa mujibu wa van Dijk (1993), nguvu na shinikizo kutoka kwa wenye uwezo hujumuishwa katika sheria na miiko na huchukua mfumo wa hejemoni. Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi hutazamia kubainisha mahusiano ya uwezo na huweka wazi majukumu ya diskosi katika kuzalisha au kupinga matumizi mabaya ya mamlaka. Nembo hii iliwashinikiza vijana kwa njia ambayo si ya moja kwa moja kutumia huduma za kampuni ya *Safaricom* badala ya kampuni nyingine yenye kutoa huduma za mawasiliano.

**Mahusiano baina ya Hadhira na Mtu Mashuhuri**

Mtu mashuhuri katika *Shujaaz* huangaziwa chini ya anwani *Celeb*. Huwa kijana mwenye wafuasi wengi ambao ni vijana wenzake na amepitia maisha yenye changamoto na akafaulu. Aidha, ni gwiji katika uimbaji, upigaji picha, uigizaji na uchekeshaji. Mtu mashuhuri hueneza masuala yenye chembechembe za imani za kiitikadi katika jarida la *Shujaaz*. Ni kupitia kwa mahojiano na mtu mashuhuri ndipo jarida hili huthibitisha kuendeleza kwa malengo na dhamira yake kuu. Kwa mujibu wa Sturken na Cartwright (2001), kiitikadi, vikatuni ni njia ambayo itikadi huzaliwa na kusawiriwa katika jamii vinamosomwa. Pia, huangazia mitazamo ya kisiasa, huhimiza itikadi na uendelezaji mahusiano ya uwezo katika jamii (Lewis na wengine, 2008).

Muundo wa lugha katika diskosi ya *Shujaaz* ulikuza mwonoulimwengu na mitazamo mahususi kuhusu aushi ya mtu mashuhuri, ambayo ililenga kushinikiza mkondo fulani wa maisha. Mfano, umaarufu wake mwana muziki Khaligraph Jones ulimpa hadhi kubwa katika jamii kuliko vijana wengine. Hadhi hii ilisababisha apewe fursa ya kusimulia tajriba ya maisha yake kupitia mahojiano. Kwa matarajio kuwa huenda vijana wenzake wangeiga mkondo wa maisha uliohimizwa na mtu mashuhuri katika mahojiano haya. Mfano wa paneli zilizoangazia mahojiano baina ya DJ Boyie na Khalighraph Jones ni *Kielelezo 6*:

**Kielelezo 6: Shujaaz chapta #82, ukurasa 8**




Khalighraph Jones, alieleza kuwa alizaliwa katika mtaa wa mabanda wa 1961 Kayole viungani mwa jiji la Nairobi. Mahusiano ya uwezo baina ya mwana muziki huyu na vijana ni wa aina mbili; kwanza ana hadhi kuliko vijana wenzake kwa sababu ya kuwa na kipaji cha uimbaji. Anavyosema Scotton (1993), ni kuwa lugha huonyesha hadhi ya wazungumzaji katika mazingira tofauti na wao hubadili msimbo ili kukidhi mahitaji ya muktadha wa mazungumzo. Aidha, lugha ni kigezo cha kupima mamlaka walionayo watu. Pili, mwimbaji Jones, alitumia mahojiano haya kujiweka katika kiwango kimoja cha uwezo na vijana wenzake waliozaliwa katika mitaa ya mabanda kama yeye.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

Aidha, mwana muziki Jones alikuza uhalisia wa mazungumzo kwa kutaja mtaa wa mabanda ambao upo katika ulimwengu wa uhalisi. Alitumia hadhi ya kuwa *Celeb* katika jamii kuwashauri vijana kuhusu mada mbalimbali. Tazama *Kielelezo 7*:

**Kielelezo 7: Shujaaz chapta #82, ukurasa 9**




*DJ Boyie: Unaweza show mafans ujanja gani iki-come mambo na Biz Unaweza washauri vipi mashabiki kuhusu masuala ya (kuanzisha) biashara.*

*Khalighraph Jones: Kuwa na ka-plan ya kile kitu unataka kufanya ndo opportunity ya doo ikijipa uko tayari. Usipate na dooh ndio uanze kufikiria ni hustle gani utaziweka.*

*Kuwa na mpango wa kile kitu unataka kufanya (ili) baadaye ukipata pesa uwe umejiandaa. Usije ukapata pesa ndio uanze kufikiria utakapowekeza.*

Ushujaa wa mtu mashuhuri panelini unatokana na ushauri kuhusu namna ya kuanzisha biashara ili kuvumbua njia mbalimbali za kujiajiri miongoni mwa vijana. Umaarufu wake wa kuwa mwana muziki miongoni mwa vijana nchini Kenya na huenda wakafuata ushauri wake bila ya kupinga. Kwa mujibu wa van Dijk (2004), lugha kama chombo cha diskosi huwa na jukumu kubwa katika kuleta mageuzi kuhusu mada fulani, maudhui na maoni. Mtu mashuhuri katika kielelezo na.7 anapendekeza mtazamo uliopaswa kukumbatiwa na vijana katika kuanzisha biashara. Vijana wanahimizwa kuwa, hatua ya kwanza katika mchakato wa kuanzisha biashara ni kuwa na pendekezo la biashara.

## Mahusiano ya Kiuana

Data ya utafiti huu ilidhihirisha mahusiano ya uwezo baina ya uana. Hii ni licha ya vikatuni vya mashujaa kuwepo ulimwenguni kwa muda wa robo tatu za karne, aghalabu vimeendelea kuibagua jinsia ya kike (Covich, 2012). Kwa mujibu wa Fairclough (1989), masuala ya kawaida katika jamii yanapowekwa katika diskosi huwa mhimili wa machukulio ya kiitikadi na huendeleza mahusiano ya uwezo. Ina maana kuwa diskosi ni zaidi ya mazungumzo na hubainika katika mawasiliano ya ishara; matendo na muktadha wa mazungumzo (Gee, 2010). Kwa mfano namna watu wanavyovaa ni sehemu ya uwasilishaji wa kiishara wa diskosi.

Naye Butler (1999) anaeleza kuwa uana ni zao la diskosi linalokuzwa na kupewa maana kupitia lugha. Matendo ya kijamii na mawasiliano baina ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

wanajamii, hubainisha uana na huafikiana na matarajio ya kijamii katika kipindi maalumu cha kihistoria (Connel, 2005). Namna wahusika katika diskosi ya *Shujaaz* walivyoshiriki katika shughuli za kiuana ni zao la kijamii la uelewaji wa uana katika muktadha wa kitamaduni, bali si kutambuliwa kuwa katika jinsia mahususi.

Diskosi ya *Shujaaz* huundwa kimakusudi kwa kuwasawiri wanaume na wanawake kuwa katika nafasi tofauti katika muundo wa kijamii. Hali hii huchangia athari hasi katika uundaji wa jamii yenye usawa wa kijinsia (Rezanova na Kogut, 2015). Kwa mujibu Fairclough (1995), diskosi hupata maana kulingana na muktadha na tajriba ya kihistoria na huegemea mtazamo ambao hujumuisha kubaguliwa katika jamii mahususi. Data ya utafiti huu ilidhihirisha mahusiano ya uwezo ya kiuana ambayo ni pamoja na: kubagua kupitia machukulio ya kijamii, kubagua kutokana na vyeo na kubagua kutokana na uwasilishwaji katika shughuli.

**Kubagua kwa Kujumuisha na Kutenga**

Diskosi husheheni masuala ya kijamii, hivi kwamba haiundwi tu bali huendeleza na kuzalisha imani (Fairclough na Wodak, 1997). Lugha huwasilishwa kupitia diskosi. Matumizi yake si tu elementi muhimu ya mawasiliano bali ni sehemu ya ushahidi wa kubainisha uana kupitia utambulisho, mahusiano, mamlaka na tabaka ili kuwasilisha ulimwengu na kinachoendelea (Leeuwen, 2008). Kwa mfano katika data ya utafiti huu wanawake walijumuishwa na kutengwa katika uraibu wa uvutaji wa sigara. Tazama *Kielelezo 8*:

**Kielelezo 8: Shujaaz chapta #88, ukurasa wa 15**




*Wife material ana-smoke!*

*Mke (anayefaa) huvutasigara! (?)*

Swali panelini lilijibiwa na mashabiki wa DJ Boyie katika mtandao wa kijamii wa *Facebook.* Ingawa, wahusika wa jinsia ya kike wamejumuishwa kupitia "mke". Lengo la nukuu hii panelini ni kumtenga mwanawake kwa kusisitiza masuala hasi kumhusu, yaani jinsia ya kike haipaswi kuvuta sigara. Swali hili lilikuwa anwani ambayo ilivutia makini ya msomaji, ikashinikiza mtazamo mahususi na baadaye ufasiri wake (van Dijk, 1988). Uteuzi wa mada hii uliongoza diskosi ya vijana katika jamii husika kuhusu suala la uvutaji wa sigara miongoni mwa wanawake.Walioshiriki katika kujibu swali, wanne ni wa jinsia ya kiume na mmoja ya kike. Waliojibu walisawiriwa kama mashujaa wanaowakomboa wanawake dhidi ya uvutaji wa sigara. Wahusika wanawake walisawiriwa kuwa dhaifu na walihitaji kukombolewa na mhusika shujaa wa jinsia ya kiume (Stabile, 2009).

Hivyo jamii inayowakilishwa katika jarida hili ilikuwa tayari kukubali wanaume kuvuta sigara ila iliwabeza wanawake wenye uraibu wa kuvuta

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

sigara. Kwa mujibu wa Wodak (1997), mfumo wa mtagusano katika jamii una jukumu la kimsingi la kuweka wazi namna wanaume na wanawake hutangamana kulingana na jinsia yao katika jamii. Uchanganuzi wa paneli ulitathmini namna lugha ilivyotumiwa katika kusawiri nafsi na ishara nyingine. Hivyo, kufafanua mahusiano ya uwezo ya kijamii katika kubainisha ni nani mwenye mamlaka ya kupinga uvutaji wa sigara kwa wanawake.

**Kubagua Kupitia Machukulio ya Kijamii**

Machukulio ya kijamii ya kiuana hudunisha dhamana ya wanawake na wasichana kwa kuegemea sana umuhimu wa wanaume na wavulana katika jamii (Michel, 1986). Kwa mujibu wa Ngari (2013), wanawake hufafanuliwa katika jamii kwa kurejelea machukulio ya kijamii. Mfano, wanaofanya kazi za nyumbani, mama, dada, wategemezi na wenye kutongoza. Naye Deem (1998) anaeleza kuwa hulka yoyote katika jamii hunasibishwa na jinsia ya kike au kiume. Msisitizo katika vikatuni huwa katika umbo la wahusika wa jinsia ya kike wala si mafanikio mengine maishani (Brown, 2011). Hii ni kwa sababu diskosi ni mwangwi wa tamaduni (Jafari, 2012), na diskosi ya vikatuni husheheni utamaduni wa jamii vinamosomwa (White na Abel, 1963).

Katika diskosi ya *Shujaaz* uchanganuzi wa machukulio ya kiuana yaliangazia majukumu yaliyotwikwa kwa kinachoonekana kama jinsia ya kweli. Kutokana na mitazamo ya uanaume na ujanajike. Wanawake walisawiriwa kuwa wa: kutongoza wanaume, kulia ovyoovyo, kutumbuiza, kuamuliwa wa kupenda na kupapaswa na wanaume bila hiari yao. Machukulio ambayo yalichangia uhalalishaji wa nafasi ya wanawake kama wategemezi, hivyo kuendeleza ukosefu wa usawa wa kijinsia katika jamii (Michel, 1986). Tazama *Kielelezo 9*:

**Kielelezo 9: Shujaaz Chapta #104, ukurasa wa 5**




Kwa mujibu wa Cocca (2014) wanawake wamewasilishwa kama chombo cha kuwavutia wanaume vikatunini kwa takribani miongo mitatu. Sehemu nyeti za maumbile yao huwekwa hadharani kimakusudi ili ziwe vivutio kwa wahusika wanaume. Mhusika wa jinsia ya kike wa pili kushoto panelini alivalia nguo zilizombana na zilizowacha sehemu za mwili nje kama vile kitovu. Kwa mujibu wa Fairclough (1995), Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi hurejelea utamaduni, jamii na itikadi ambayo hubainisha maana ya diskosi. Matendo na mawasiliano ya mhusika wa jinsia ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

kike panelini yalipangwa na kuandaliwa kiuana. Yaliafikiana na mawazo na matarajio ya muktadha wa kijamii katika kipindi maalumu cha kihistoria. Mhusika wa jinsia ya kike anasema:

> *Uuuuuhhh Man-Like uko poa!*
>
> *Uuuuuhhh (!) (mshangao) Man-Like Kalito unapendeza.*

Nukuu hii ilithibitisha kuwa mhusika mwanamke alivutiwa kimapenzi na Man-Like Kalito. Kwa mujibu wa van Dijk (2009), diskosi haiangazii muundo wa diskosi pekee bali namna usemi unavyozalishwa na kikundi au watu mahususi. Hivyo, uzalishaji na uelewaji wa diskosi hudhibitiwa na muktadha. Mhusika wa jinsia ya kike kuvutiwa na Man-Like Kalito ni zao la kijamii katika uelewaji wa uana katika muktadha wa kitamaduni, bali si tu kutambuliwa kuwa katika jinsia ya kike. Mwanamke alisawiriwa kama mwenye kutongoza wanaume. Hivyo anadunishwa kwa sababu ya uana, yaani mwanamke.

**Ubaguzi Kutokana na Vyeo**

Diskosi huathiriwa na jamii ambayo hudhihirisha suala muhimu la mamlaka (Wodak na Meyer, 2008). Mamlaka ambayo hayazalishwi na diskosi (Weiss na Wodak, 2003), bali diskosi hujukumika kama chombo cha kueleza, tofauti ya mamlaka katika miundo ya kijamii (Wodak na Meyer, 2008). Diskosi ya *Shujaaz* haina mahusiano ya uwezo ya kiuana kivyake bali inapata mamlaka haya inapotumika na watu wenye mamlaka katika muktadha wa jamii unaowabagua wahusika wanawake (Weiss na Wodak, 2003). Mahusiano ya uwezo ya kiuana yalidhihirika kupitia kubaguliwa kwa wanawake katika vyeo vya kisiasa na kiutawala. Wanaume waliwasilishwa kama wawakilishi wa wadi, magavana na machifu. Mwanawake aliwasilishwa kwa mfano kama mke wa chifu na hadhira ya mwanasiasa wa jinsia ya kiume. *Kielelezo 10* kina mhusika mwanaume kama kiongozi:

**Kielelezo 10: Shujaaz Chapta #97, ukurasa wa 22**




> *So sahii wamekuwa kwa ofisi more than half a year. Leo ningependa kujua tu kwa maoni yako ni kazi gani **gavana** anafaa kuwa anafanya.*

> *Wakati huu wamekuwa kwenye ofisi kwa muda unaozidi nusu mwaka. Leo ningependa kujua maoni yako kuhusu majukumu ya gavana.*

Gavana katika kauli hii ni mhusika anayetumia kipaza sauti. Ingawa, viongozi wa jinsia ya kiume

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946


wamesawiriwa kama wasiotimiza ahadi na wanaotumia utapeli kupata uongozi. Wahusika wanawake hawajapewa nafasi ya uongozi hasa wa kisiasa au kiutawala. Fairclough na Wodak (1997), wanaeleza kuwa diskosi huathiri jamii na utamaduni. Vilevile, jamii na utamaduni huathiri diskosi. Wanawake walipuuzwa kutokana na utamaduni uliowabagua. Kwa mujibu wa Fairclough na Wodak (1997), Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi hurejelea utamaduni, jamii na itikadi ambayo hubainisha maana na athari za diskosi. Mahusiano ya uwezo ya kiuana yalidhihirika kupitia mtagusano baina ya mhusika mwanaume ambaye ni kiongozi na wanawake ambao ni watawaliwa. Hivyo, diskosi hii ni kifaa cha mahusiano baina ya makundi ya matabaka au miundo mingine ya kijamii au baina ya watu kama wanachama wa kundi la kijamii (van Dijk, 1989). Huenda ndio sababu wahusika wanawake wamewasilishwa panelini kuwa miongoni mwa hadhira.

Diskosi ya *Shujaaz* iliibagua jinsia ya kike katika vyeo kwa kuendeleza mahusiano ya uwezo ya uana yaliyowasawiri wanawake kama kundi linalotawaliwa. Wodak (2004), anasema kuwa namna diskosi inavyowakilisha nafasi ya washiriki, huzalisha mahusiano ya uwezo yasiyokuwa na usawa. Uchanganuzi wa paneli ulidhihirisha muundo usiowazi katika uwasilishaji wa uana. Jinsia ya kike ilibaguliwa katika uongozi wa kisiasa au kiutawala.

**Kubagua Kutokana na Uwasilishwaji katika Shughuli**

Vikatuni huleta watu pamoja au kuwatenganisha (Lewis na Wengine, 2008). Shughuli ambazo jinsia ya kike ilitengwa katika data ya utafiti ni pamoja na: uvumbuzi wa vifaa mbalimbali, ufundi wa kieletroniki, uchezaji wa mpira na uchawi. Tazama *Kielelezo 11:*

**Kielelezo 11: Shujaaz Chapta #100, ukurasa wa 13**




Anavyosema van Dijk (1996), ni kuwa mamlaka ya kijamii ni mchakato unaodhibiti kundi moja au shirika dhidi ya matendo ya wanachama wake au akili za wanachama wa kundi tofauti. Mamlaka haya huzuia uhuru wa matendo ya wengine au kushinikiza maarifa, mielekeo na itikadi yao. Wanaoshiriki katika mchezo wa kandanda katika kielelezo na.11 ni wahusika wa jinsia ya kiume.

Wahusika wanawake walibaguliwa kwa kutowasilishwa katika shughuli zilizohitaji maarifa na ujuzi. Ni upeo wa Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi katika muktadha huu kuangazia matumizi ya diskosi katika kuwasilisha mifumo isiyokuwa na usawa na iliyoendeleza udhalimu dhidi ya jinsia ya kike. Suala la uana halijatupiliwa mbali. Kushiriki katika shughuli hizi hurithishwa katika kipindi cha

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

kuzaliwa na huumbwa kulingana na mazoea na michakato ya kijamii kila wakati. Katika data ya utafiti huu wanawake waliwasilishwa kama watazamaji tuli na wanaume kama watendaji wa shughuli. Shughuli walizopewa wanaume zilikuwa za kijasira na kufurahisha ilhali shughuli za wanawake zilikosa ubunifu na uvumbuzi na zilihusu masuala ya kiujumi.

## HITIMISHO

Makala hii ilitathmini mahusiano ya uwezo yalivyowasilishwa katika diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*. Mhimili wa nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi unaoeleza kuwa diskosi husheheni mahusiano ya uwezo ulikuwa nguzo muhimu katika uchanganuzi wa data. Ilidhihirika kuwa mahusiano ya uwezo yaliwasilishwa kupitia: Mahusiano ya uwezo baina ya mashujaa wahusika na wahusika wa kawaida, wahusika mashujaa na vijana, wadhamini na vijana, mahusiano ya uwezo ya kiuana na hadhira na mtu mashuhuri. Vikatuni vya *Shujaaz* vilibainika kuwa chombo anachotumia mwandishi na wadhamini kuzalisha uwezo katika muktadha wa vijana ili kuwadhibiti kama kundi tawaliwa nchini Kenya. Uwezo huu ulidokezwa na itikadi iliyowalazimu vijana kuhusiana kwa njia ya kipekee na wanajamii wengine kulingana na kikundi chao katika jamii. Makala hii inapendekeza tafiti zaidi za baadaye zifanywe kwa kuzingatia mikakati ya uhalalishaji na uharamishaji inayodhihirika kupitia mahusiano ya uwezo katika diskosi ya *Shujaaz*.

## MAREJELEO


Alvi, S. D., & Baseer, A. (2012). An Analysis of Barak Obama’s Speech the Great Need of Hour, in: *Interdisciplinary Journal of Contemporary*, Research in Business 319, 617-635.

Beck, M. R. (1999). *Comics in Swahili or Swahili Comic*? AAP 60 (1999) 67-101.

Boyd, J. (2015). *Racializing in Comic Books: An Examination of Marvel Comics the Punisher* (2004) St. Mary’s University, Halifax, Nova Scotia.

Brown, J. A. (2011). *Black Superheroes, Milestone Comics and the Fans*, University Press, Mississipi University.

Butler, J. (1999). *Gender Trouble: Feminism and the Subversion of Identity (10th Anniversary ed)*. New York and London: Routledge.

Cocca, C. (2014). The Broke Back Test: A Quantitative and Qualitative Analysis of Portrayals of Women in Mainstream Superhero Comics, 1993-2013, *Journal of Graphic Novels na Comics*, 5(4) page 411-428.

Connel, R. W. (2005). *Masculinities (2nd)*, Crows Nest N.S.W: Allen & Unwin.

Covich, A. R. (2012). Alter/Ego: Superhero Comics Books Readers Gender and Identities. (Unpublished MA Thesis). University of Canterbury.

Deem, R. (1998). *Women and School*. London: Routledge na Kegan Paul.

Dittmer, J. (2005). Captain America’s: Reflection on Identity, Popular Culture and Post 9/11 Geopolitics, *Annals of the Association of American Geographer*, 95(2) 624-643.

Eagleton, T. (1991). *Ideology: An Introduction*. London: Verso.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*, New York: Longman.

Fairclough, N. (1992). Discourse and Text. Linguistic Intertextual Analysis within Discourse analysis, in: *Discourse and society*, SAGE Publication Limited, California: 3:193-217.

Fairclough, N. (1995). *Critical Discourse Analysis: The Critical Study of Language*, London: Longman.

Fairclough, N. & Wodak, R. (1997). Critical Discourse Analysis. In Ed. Van Djik, T. *Discourse Studies*: A *Multidiscplinary Introduction*. pp 258-284. London: Sage.

Gay, M. (1992). *Educational Research: Competence for Analysis and Application (3rd edition)*, Meril Publishing Company, Idianopolis, Indiana: USA.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946


Gee, J. P. (2005). *An Introduction to Discourse Analysis: Theory and Method*, (2nd ed, New York, NY: Routledge.

Gee, J. P. (2010). *An Introduction to Discourse Analysis: Theory and Method*, Taylor na Francis.

Githiora, C. (2002). Sheng: Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? In: *Journal of African Cultural Studies*. 5(2),pg 159-181.

Ivan, R., & Clark, R. (1997). *Writing and Identity: Discourse Construction of Identity in Academics*, John Benjamin Publishers.

Jafari, S. M. (2012). *Language and Culture*. 2(17), 230-235.

Jigal, B. (2006). Stupid Hares and Margarine: Early Swahili Comics in: L. John, *Cartooning in Africa*, Cresskill: Hampton Press.

Kading, T. (2005). Drawing into 9/11, but where have all the Superheroes Gone, in Mclaughin (ed) *Comics as Philosophy*, University Press of Mississipi, Jackson.

Kothari, C. R. (2009). *Qualitative Technique*, 3E. Vikas Publishing House PVT LTD.

Lanternari, V. (1970). Comics and Caricatures in Non- European Cultures: Africa, in: *Encyclopeadia of World Art*, New York: McGrow-Hill.

Lent, J.A. (2009). *African Cartooning: An Overview of Historical and Contemporary Issues*, Cresskill, NJ: Hampton Press.

Lewis, V. & Wengine (2008). The Muhammad Cartoons and Humor Research: A Collection of Essays in: *Humor: International Journal of Humor Research*, 21(1). 1-46.

Michel, A. (1986). *Down with Stereotypes: Eliminating Sexism from Children's Literature and School Textbook*, Paris: UNESCO.

Mikkonen, K. (2017). The narratology of Comic Art, in: *Routledge Advance in Comic Studies*, Routledge: New York: USA.

McCloud, S. (1993). *Understanding Comics: The Invisible Art*, Northampton MA: Kitchen Sink Press.

Mugenda, O. M., & Mugenda, G. A. (1999. *Research Methods: Quantitativeand Qualitative Approaches.* nairobi; Acts Press.

Nesler, M. S. & Wengine (1981). The Effect of Credibility on Perceived Power, *Journal of Applied Social Psychology*, 23(17), 1407-25.

Ngari, P. K. (2013). Portrayals of Women in Kenya Television Advertisement, (M.A Thesis, Unpublished), The University of nairobi, nairobi: Kenya.

Ngugi, P. (2017). Fasihi katika Lahaja Ibukizi. Mifano kutoka Chapisho la *Shujaaz*, katika *Mulika*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Toleo maalumu la Makala ya Kongamano la CHAUKIDU ukurasa wa 57-64.

Nortion, B. (2003). *The Motivation Power of Comic Books: Insight from Archie Comics Readers*, The Reading Teacher, 57(2), page 140-147.

Nyberg, A. K. (1998). *Seal of Approval: The History of Comics Code*, University Press of Mississipi, Mississipi, USA.

Otuoma, D. A. (2015). Mitindo na Maudhui katika Uchanganuzi wa Vibonzo kwenye Gazeti la Taifa Leo (Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa), Chuo Kikuu cha nairobi.

Phillips, N. D. & Strobl, S. (2006). *Cultural Criminology and Kryptonite*: Apocalyptic and Retributive Constructions.

Raskin, V. (2008). On Political of Humour, Humour: *International Journal of Humor Research* 21(1), 26-30.

Rezanova, Z. I., & Kogut, S. V. (2015). Types of Discourse Marker: Their Ethnocultural Diversity in Scientific Text. *Procedia-social and Behavioral Science*, 215: 266-272: https://doi.org/10.1016/j.sbspro.2015.//.633, retrieved on 28.1.2021.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.946

Sardabi, F., Biria, R., & Azin, N. (2014). Rouhan's UN speech: A Change in Ideology or Strategy, *International Journal of Language Learning and Applied Linguistics world*, 7(3), 84-97.

Scotton, C. M. (1993). *Social Motivation for Code Switching – Evidence from Africa*, Oxford; Clarendon.

Scott, C. A. (2007). Written in Red, White, and Blue: Comic Book Propaganda from World War II and 9/11, *Journal of Popular Culture 381*, #2.

Scott, C. A. (2011). Comic and Conflict: War and Patriotically Themed Comics in American Cultural History from World War II Through the Iraq War, (Unpublished PhD Theses) Loyola University, Chicago, USA.

Stabile, C. A. (2009). Sweetheart, this ain't Gender Studies: Sexism and Superheroes, *Communication and Critical Cultural Studies*, 6(1), page 86-92.

Sturken, M., & Cartwright, L. (2001). *Practices of Looking: An Introduction to Visual Culture*. New York: Oxford University Press.

van Dijk, T. A. (1987). *Discourse and the Reproduction of Racism*, University of Amsterdam. Centre for Race and Ethnic Studies.

van Dijk, T. A. (1988). *News as Discourse*, New York and London: Routledge.

van Dijk, T. A. (1989). Structure and Strategies of Discourse and Prejudice, *Ethnic Minorities Journal*, Amsterdam: Swetsy Zitlinger.

van Dijk, T. A. (1993). Principles of Critical Discourse, *Discourse and Society*; 4(2) 249-283.

van Dijk T. A. (1996). Discourse Power and Access, in: C. Coulthard & M. Coulthard (Eds). *Text and Practices: Reading in Critical Discourse Analysis*. Pg 84-104, London: Routledge.

van Dijk, T. A. (2001). Critical Discourse Analysis, in D. Schiffrin, D. Tannen and H.E. Hamilton (Eds) *Handbook of Discourse Analysis*. Oxford: Blackwell.

van Dijk, T. A. (2004). "From Text Grammar to Critical Discourse Analysis", *Working Paper*. Barcelona: Universitat.

van Leeuwen, T. (2008). *Discourse and Practice*: New Tool for Critical Discourse Analysis, New York: Oxford University Press.

van Dijk, T. A. (2009). How Social Contexts Influence Text and Talk in: *Society and Discourse*, Cambridge: Cambridge University Press.

Weiss, G., & Wodak, R. (2003). Theory, Interdisciplinary and Critical Discourse Analysis in: G. Weiss & R. Wodak (Eds), *Critical Discourse Analysis: Theory and Interdisciplinary*, pp 1-34, Hamshire: Pagrave Macmillan.

White, D., & Abel, H. (1963). *The Funnies: An American Idiom*, London: The Free Press of Glenceo.

Wertham, F. (1954). *Seduction of the Innocent*, Rinerhart & Company, USA.

Wodak, R. (1997). *Gender and Discourse*, California: Sage Publication.

Wodak, R. (2004). Critical Discourse Analysis. In C. Seale, G. Gobo, J. Gubrium, & D. Silverman (Eds.), *Qualitative Research Practice*, (pp. 185-201). London: Sage Publications.

Wodak, R., & Meyer, M. (2008). Critical Discourse Analysis: History, Agenda, Theory, and Methodology in: *Methods for Critical Discourse Analysis*, (Second, pp. 1-33). London: Sage.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.